# SAYANSI JAMII

## 1.0 UTANGULIZI

Muundo wa mtihani huu umetayarishwa kuwaongoza watahini jinsi ya kutunga maswali ya mtihani. Muundo huu unajumuisha mada zilizomo katika muhtasari wa mwaka 2022 kuanzia Darasa la V, VI na VII. Malengo ya jumla, ujuzi na maudhui ya mtihani yaliyomo humo yanatokana na muhtasari wa somo la Sayansi Jamii uliotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA-2022) Zanzibar.

## 2.0 MATOKEO YA JUMLA

Matokeo ya jumla yatakayopimwa katika mtihani wa Sayansi Jamii yatahusisha mwanafunzi kuonesha uwezo wa:

**2.1** Kueleza na kuthamini historia ya nchi yake, utaifa, haki za binadamu na uzalendo.

**2.2** Kutumia tabia, maadili, tamaduni na itikadi zinazokubalika katika maisha yake ya kila siku.

**2.3** Kuelezea matukio muhimu ya kihistoria ya Zanzibar na katika ulimwengu, kuishi kulingana na kanuni za kijamii, kupambana na rushwa kikamilifu kwa maendeleo ya jamii.

**2.4** Kuchambua maeneo ya umbile ya kijografia ya Zanzibar.

## 3.0 MALENGO YA JUMLA

Malengo ya jumla ya mtihani wa Sayansi Jamii ni kupima yafuatayo:-

**3.1** Kuelezea uhusiano kati ya wazanzibari na jamii za nje kabla ya 1800.

**3.2** Kuelezea hatua alizopitia mwanadamu katika kupambana na mazingira yake katika nyakati mbali mbali za kimaisha.

**3.3** Kutumia elimu ya uraia katika kujenga afya, nidhamu, haiba na uaminifu kwa wanajamii.

**3.4** Kutumia maktaba na vifaa vya TEHAMA kwa usahihi ili kupata maarifa na stadi za kiraia na Sayansi jamii.

**3.5** Kuelezea misingi ya demokrasia, utawala bora na dhana ya uzalendo katika kujenga raia wema.

**3.6** Kuelezea miundo ya serikali ya Mapinduzi Zanzibar na serikali ya Juamhuri ya Muungano wa Tanzania na uendeshaji wake.

**3.7** Kubainisha Jumuiya za kimataifa ambazo Tanzania ni mshiriki na kutathmini manufaa ya ushirika huo.

**3.8** Kutumia mazingira halisi, picha na ramani kuelezea Jografia ya Zanzibar na dunia kwa ujumla.

## 4.0 MUUNDO WA MTIHANI

Kutakuwa na mtihani mmoja wenye muda wa saa mbili na nusu (2.30) na kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu utafanywa kwa muda wa saa tatu (3:00). Mtihani huu utakuwa na sehemu tatu (3) **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na moja (11). Mwanafunzi atatakiwa kujibu maswali tisa (9). Mtihani huu utakuwa na alama 100.

### 4.1 SEHEMU A: (Alama 30)

Sehemu hii itakuwa na maswali matatu **(1- 3)**, swali la kwanza la kuchagua jawabu sahihi lenye vipengele kumi (10), kila kipengele kitakuwa na alama moja (01) na kulifanya swali hilo kuwa na alama kumi (10). Swali la pili litakuwa na vipengele kumi (10) vya maswali ya kweli/sikweli, kila kipengele kitakuwa na alama moja (01) na kulifanya swali hilo kuwa na alama kumi (10). Swali la tatu litakuwa la kuoanisha na litajumuisha vipengele vitano (5) vyenye alama mbili (2) kila moja, hivyo kuwa na jumla ya alama kumi (10).

### 4.2 SEHEMU B: (Alama 40)

Sehemu hii itakuwa na maswali manne **(4 – 7)**, katika sehemu hii maswali yake yatakuwa ya majibu mafupi, ambayo yatakuwa na vipengele vitano (5) kwa kila swali na kila kipengele kitakuwa na alama mbili (2) na kufanya kila swali kuwa na alama kumi (10).

## 4.3 SEHEMU C: (Alama 30)

Sehemu hii itakuwa na maswali manne **(8 - 11),** ambayo yatakuwa ni ya kueleza. Mtahiniwa atatakiwa kujibu maswali mawili (2) ambapo kila swali litakuwa na alama kumi na tano (15).

## 5.0 MADA ZITAKAZOTAHINIWA

**5.1** Nchi yetu Zanzibar
**5.2** Historia ya Zanzibar kabla ya mwaka 1800
**5.3** Mfumo jua
**5.4** Mifumo ya kijamii duniani
**5.5** Elimu ya uraia
**5.6** Ramani
**5.7** Biashara ya utumwa Zanzibar
**5.8** Nchi za Afrika mashariki
**5.9** Shughuli kuu za kiuchumi Zanzibar
**5.10** Usafiri na mawasiliano
**5.11** Idadi ya watu na makaazi Zanzibar
**5.12** Tanganyika kabla, wakati na baada ya ukoloni
**5.13** Uhusiano baina ya Zanzibar na nchi za Asia
**5.14** Uhusiano baina ya Zanzibar na nchi za ulaya
**5.15** Utawala wa Oman Zanzibar
**5.16** Harakati za kudai uhuru Zanzibar
**5.17** Ukoloni mamboleo na Utandawazi
**5.18** Mabara na Bahari
**5.19** Uatawala wa Kiingereza Zanzibar
**5.20** Serikali
**5.21** Uzalendo
**5.22** Demokrasia na Utawala bora
**5.23** Jumuuiya ya Afrika Mashariki
**5.24** Uhusiano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya za Kimataifa
**5.25** Mali asili za Afrika Mashariki.

## 6.0 JADWELI LA KUTAHINI

| | | Nyanja za utambuzi | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Mada** | **Kukumbuka** | **Kufahamu** | **Kutumia** | **Kuchambua** | **Kutathmini** | **Kuunda** | **Idadi ya maswali** | **Asilimia kwa kila mada** |
| 1. | Nchi yetu Zanzibar | | | | | | | **2** | **4** |
| 2. | Historia ya Zanzibar kabla ya mwaka 1800 | | | | | | | **2** | **4** |
| 3. | Mfumo jua | | | | | | | **2** | **4** |
| 4. | Mifumo ya kijamii duniani | | | | | | | **1** | **2** |
| 5. | Elimu ya uraia | | | | | | | **2** | **5** |
| 6. | Ramani | | | | | | | **1** | **2** |
| 7. | Biashara ya utumwa Zanzibar | | | | | | | **2** | **3** |
| 8. | Nchi za Afrika mashariki | | | | | | | **2** | **4** |
| 9. | Shughuli kuu za kiuchumi Zanzibar | | | | | | | **3** | **7** |
| 10. | Usafiri na mawasiliano | | | | | | | **2** | **3** |
| 11. | Idadi ya watu na makaazi Zanzibar | | | | | | | **2** | **5** |
| 12. | Tanganyika kabla, wakati na baada ya ukoloni | | | | | | | **5** | **10** |
| 13. | Uhusiano baina ya Zanzibar na nchi za Asia | | | | | | | **2** | **3** |
| 14. | Uhusiano baina ya Zanzibar na nchi za ulaya | | | | | | | **2** | **3** |
| 15. | Utawala wa Oman Zanzibar | | | | | | | **2** | **3** |
| 16. | Harakati za kudai uhuru Zanzibar | | | | | | | **2** | **5** |
| 17. | Ukoloni mamboleo na utandawazi | | | | | | | **1** | **2** |
| 18. | Mabara na bahari | | | | | | | **1** | **2** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 19. | Uatawala wa kiingereza Zanzibar | | | | | | | 2 | 5 |
| 20. | Serikali | | | | | | | 2 | 5 |
| 21. | Uzalendo | | | | | | | 2 | 3 |
| 22. | Demokrasia na utawala bora | | | | | | | 1 | 2 |
| 23. | Jumuuiya ya Afrika Mashariki | | | | | | | 2 | 4 |
| 24. | Uhusiano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Jumuiya za Kimataifa | | | | | | | 2 | 5 |
| 25. | Mali asili za Afrika Mashariki. | | | | | | | 2 | 4 |
| **Idadi ya maswali kwa kila nyanja** | | | | | | | | **49** | |
| **Asilimia ya maswali kwa kila nyanja** | | | | | | | | | **100** |